


Dawa za Kuzuia Virusi za Kumeza ni Nini?



Tembe za kusaidia mtu aliyeambukizwa COVID-19 kupata nafuu.

Ukiwa katika hatari kali ya COVID-19 na umepatikana na maambukizo ya COVID-19 ndani ya siku 5 zilizopita, huenda ukataka kuzingatia kutumia tembe zilizopendekezwa za kumeza. Matibabu mawili yanapatikana: [Paxlovid™](#) (Pfizer) na [legeviro](#) (Merck). Unaweza kufuzu kupata mojawapo ya matibabu haya ya COVID-19 kutegemea umri wako, historia ya afya, na kipindi ambacho umekuwa na dalili.

Matibabu ya dawa za kukinga virusi yanaweza kusaidia mwili wako kupigana na COVID-19 kwa kuzuia virusi vya SARS-CoV-2 (virusi vinavyosababisha COVID-19) dhidi ya kuzaana na kuongezeka mwilini mwako, kuzuia kiwango cha virusi ndani ya mwili wako, au kusaidia mfumo wako wa kingamwili. Kwa kupata matibabu, unaweza kuwa na dalili hatari kiasi na yanaweza kupunguza nafasi za matibabu yako ya kuwa hatari na kuhitaji utunzaji hospitalini.

• NITAMEZAJE DAWA HII YA KUKINGA VIRUSI?

Kupata matibabu ya kumeza ya kuzuia virusi kunamaanisha utakuwa unameza tembe. Unafaa kutumia dawa za kumeza za kuzuia virusi ulivyoagizwa na mhudumu wako wa afya. Usiruke dozi au kutumia dozi za ziada utakapokosa dozi. Unafaa kutumia dawa zote ulivyoelekezwa hadi utakapozimaliza au mhudumu wako wa afya atakapokuambia uache. Dawa za kuzuia virusi zinaweza kutumiwa pamoja na chakula au bila chakula na inapendekezwa kuwa tembe hizo zimezwe mzima, bila kuzivunja au kuzisaga.


• JE, NIKIWA NA HALI ILIYOPO YA AFYA KAMA VILE SHIDA ZA FIGO NA MAINI?

Kabla ya kutumia dawa yoyote, unafaa kujadili historia yako ya afya na mhudumu wako wa afya. Hii inajumuisha kuwaambia kuhusu hali zozote za afya ambazo tayari umekuwa nazo na dawa zilizopendekezwa, dawa za kununua kwa maduka, vitamini, na viziada unavyotumia.

Watu walio na matatizo yoyote ya figo au maini wanafaa kuongea na mhudumu wao wa afya kuhusu hali yao kabla a kutumia matibabu ya dawa ya kuzuia virusi. Mhudumu wako wa afya anaweza kuamua iwapo matibabu ya kuzuia virusi ni sawa kwako na iwapo dozi yako ni sawa. Baadhi ya matibabu huenda yasipendekezwe kwa watu walio na hali fulani.

- **JE, NA IWAPO SITAFUZU KUPOKEA MATIBABU YA KUMEZA YA KUZUIA VIRUSI?**

Mhudumu wako wa afya anaweza kuamua kuwa hufuzu kupokea matibabu ya kuzuia virusi au yaliyosahihi kwako. Huenda kuna sababu kadhaa kwa hili. Huenda usitimize vigezo vyote vya kustahiki, au huenda una hali ya afya ambayo huenda isiwe sawa kwa matibabu fulani. Jadili chaguo za matibabu bora kwako na kwa mhudumu wako wa afya.



DOH 825-029 May 2022 Swahili

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe kwa <mailto:ecivil.rights@doh.wa.gov>.